**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA SABA**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA**

**10 MEI, 2017**

## MKUTANO WA SABA

## KIKAO CHA ISHIRINI NA MOJA TAREHE 10 MEI, 2017

### I. DUA:

Saa 3:00 asubuhi Mhe. Tulia Ackson (Naibu Spika) alisoma dua na kuongoza Kikao cha Bunge.

**Makatibu Mezani:**

1. Ndugu Ramadhan Issa
2. Ndugu Asia Minja
3. Ndugu Zainab Issa

### II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani:-

1. Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambayo iliwasilishwa na Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

2. Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliyowasilishwa kwa niaba ya Mwenyekiti na Mhe. Ali Khamisa Mattar.

3. Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maji na Umwagiliaji juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 iliwasilishwa Mezani na Mhe. Cecil David Mwambe.

## III. MASWALI

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI)

Swali Na. 175: Mhe. Juliana Daniel Shonza

Nyongeza: Mhe. Juliana Daniel Shonza
Mhe. Freeman Aikaeli Mbowe
Mhe. Richard Mganga Ndassa

### WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI

Swali Na. 176: Mhe. Deo Kasenyenda Sanga

Nyongeza: Mhe. Deo Kasenyenda Sanga
Mhe. Saumu Heri Sakala
Mhe. Mary Michael Nagu

Swali Na. 177: Mhe. Azza Hillal Hamad (kwa niaba ya Mhe. Subira Khamis Mgalu)

Nyongeza: Mhe. Azza Hillal Hamad
Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe
Mhe. Salome Wycliffe Makamba
Mhe. Rashid Abadallah Shangazi

### WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Swali Na. 178: Mhe. Gibson Blasius Ole-Meiseyeki
Nyongeza: Mhe. Gibson Blasius Ole-Meiseyeki

Swali Na. 179: Mhe. Halima James Mdee
Nyongeza: Mhe. Halima James Mdee

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Swali Na. 180: Mhe. Shaaban Omari Shekilindi
Nyongeza: Mhe. Shaaban Omari Shekilindi

Swali Na. 181: Mhe. Boniventura Destery Kiswaga
Nyongeza: Mhe. Boniventura Destery Kiswaga

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

Swali Na. 182: Mhe. Raisa Abdallah Mussa (kwa niaba ya Mhe. Yussuf)
Nyongeza: Mhe. Raisa Abdallah Mussa

Swali Na. 183: Mhe. Taska Restituta Mbogo
Nyongeza: Mhe. Taska Restituta Mbogo

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Swali Na. 184: Mhe. Elias John Kwandikwa

Nyongeza: Mhe. Elias John Kwandikwa
Mhe. Musukuma Joseph Kasheku

## IV. MATANGAZO:

1. Wageni mbalimbali walioko kwenye *Galleries* za Ukumbi wa Bunge walitambulishwa.

2. Kikao cha CPA Tawi la Tanzania kwa Kamati ya Utendaji saa 5:00 asubuhi ukumbi Ns. 229.

3. Semina kwa Wabunge Vijana na Wabunge wa EU saa 10:00 jioni Dodoma Hotel.

4. Kikao cha TWPG Ukumbi wa zamani wa Zahanati ya Bunge saa 7:00 mchana.

5. Ratiba mpya ya Vikao vya Bunge imetolewa ambayo itakuwa na siku za Jumamosi.

**MIONGOZO**

(i) Mhe. Dkt. Immaculate Semesi Sware aliomba Mwongozo wa Spika kuhusu Vikao vya Bajeti wakati wa kushika shilingi kwenye kipindi cha Kamati ya Matumizi kwamba haitoi haki kwa Wizara husika.

Kiti kilielekeza kwamba nafasi hutolewa kwa uwiano na Wabunge wenyewe wabadilike kwenye kutumia muda huo.

(ii) Mhe. Godbless Jonathan Lema aliomba Mwongozo wa Spika kuwa Mkuu wa Shule Lucky Vincent amekamatwa na Polisi na kwanini RTO asichukuliwe hatua kwa kuwa kabla ya kufika eneo la ajali kuna *Traffic Barriers* kama nne.

Kiti kilimjibu Mhe. Godbless Jonathan Lema kwmaba, Kwa mujibu wa Kifungu 68 halijatokea Bungeni.

(iii) Mhe. Pauline Philipo Gekul, kwanini Fedha za Mfuko wa Jimbo zimepungua?

Kiti kilielekeza kwamba hakukuwa na Mwongozo uliombwa na Mhe. Pauline Philipo Gekul labda kama Waziri wa TAMISEMI atataka kulifanyia kazi suala hilo.

(iv) Mhe. Mussa Bakari Mbarouk alizungumzia mafuriko ya Tanga na kwamba Je, Serikali inawasaidia nini Wananchi wa Tanga?

Kiti kilijibu Mwongozo huo kwamba jambo hilo halijatokea Bungeni.

## V. MAELEZO YA SPIKA

Mhe. Naibu Spika alitoa maelezo ya jumla ya kuwakumbusha Wabunge juu ya matumizi ya Kifungu 68 kuwa ni vema Wabunge wakatumia Kanuni hiyo kwa mujibu wa Kanuni.

## VI. HOJA YA KUTENGUA KANUNI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Vijana, Ajira, Kazi na Walemavu) Mhe. Jenista J. Mhagama alitoa Hoja ya kutengua Kanuni kwa mujibu wa Kifungu 153 ili Bunge liweze kukutana leo saa 10:00 jioni badala ya saa 11:00 jioni. Wabunge walihojiwa na kuafiki.

## VII. HOJA ZA SERIKALI

1. Hoja ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Waziri wa Maji aliwasilisha Hotuba ya Wizara hiyo.

2. Mhe. Oliver Semuguruka kwa niaba ya Mwenyekiti aliwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji.

3. Mhe. Hamidu Bobali aliwasilisha Taarifa ya Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

   Wachangiaji wa Hoja ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

   1. Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga - CCM
   2. Mhe. Kabwe Zuberi Zitto - ACT

   Kikao cha Wabunge wote wa CCM kitafanyika White House saa 8:30.

## VIII. KUSITISHA SHUGHULI ZA BUNGE

Shughuli za Kikao cha ishirini na moja zilisitishwa saa 7:00 mchana hadi saa 10:00 jioni.

## IX. BUNGE KUREJEA

Shughuli za Kikao cha Bunge zilirejea saa 10:00 jioni na Waheshimiwa Wabunge wafuatao waliendelea kuchangia Hoja ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji.

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Mhe. Mary Michael Nagu | - | CCM |
| 4. | Mhe. Jasson Samson Rweikiza | - | CCM |
| 5. | Mhe. Matta Ali Salum | - | CCM |
| 6. | Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka | - | CCM |
| 7. | Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma | - | CCM |
| 8. | Mhe. Nape Moses Nnauye | - | CCM |
| 9. | Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka | - | CHADEMA |
| 10. | Mhe. Rose Kamil Sukum | - | CHADEMA |
| 11. | Mhe. Julius Kalanga Laizer | - | CHADEMA |
| 12. | Mhe. Tunza Issa Malapo | - | CHADEMA |
| 13. | Mhe. Magdalena Hamis Sakaya | - | CUF |
| 14. | Mhe. Mussa Bakari Mbarouk | - | CUF |
| 15. | Mhe. Suleiman Said Bungara | - | CUF |
| 16. | Mhe. Seif Said Gulamali | - | CCM |
| 17. | Mhe. Anna Richard Lupembe | - | CCM |
| 18. | Mhe. Josephine Johnson Genzabuke | - | CCM |

## X. UCHAGUZI WA WABUNGE

(a) Maelezo ya Spika:

Spika alitoa maelezo kuhusu maudhui ya uchaguzi wa EALA.

(b) Maelezo ya Msimamizi wa Uchaguzi:

Katibu wa Bunge akiwa Msimamizi wa Uchaguzi alitoa maelezo na utaratibu wa uchaguzi wa EALA ambao wagombea ni wa

Chama cha Demokrasia na Maendeleo tu ili kukamilisha Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki (EALA).

(c) Baadhi ya Wabunge wafuatao waliomba maelezo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| (i) | Mhe. George Malima Lubeleje | - | CCM |
| (ii) | Mhe. Boniface Mwita Getere | - | CCM |
| (iii) | Mhe. Stella Ikupa Alex | - | CCM |
| (iv) | Mhe. Hamidu Hassan Bobali | - | CUF |
| (v) | Mhe. Maftaha Abdallah Nachuma | - | CUF |
| (vi) | Mhe. Musukuma Joseph Kasheku | - | CCM |
| (vii) | Mhe. Joshua Samwel Nasari | - | CHADEMA |
| (viii) | Mhe. Philipo Augustino Mulugo | - | CCM |
| (ix) | Mhe. Pacal Yohana Haonga | - | CHADEMA |

(d) Maelezo zaidi ya Spika:

Mhe Spika alitoa maelezo ya zaidi kwa nini leo unafanyika uchaguzi huu.

(e) Katibu wa Bunge alitoa ufafanuzi zaidi kuhusu utaratibu wa upigaji kura utakaotumika na maandalizi yote kwa jumla.

(f) Wagombea waliitwa mmoja mmoja ili kuja kujieleza na kuomba kura kama ifuatavyo:-

(i) Prof. Abdallah Jumbe Safari – aliulizwa maswali matatu
(ii) Ezekia Dibogo Wenje – aliulizwa maswali matatu
(iii) Josephine Sebastian Lemoyan – aliulizwa maswali matatu
(iv) Laurance Kego Masha – aliulizwa maswali matatu
(v) Pamela Simon Maassay – aliulizwa maswali matatu
(vi) Salum Mwalim Juma – aliulizwa maswali matatu

(g) Spika aliongeza muda hadi zoezi la uchaguzi na kuhesabu kura litakapomalizika.

(h) Utaratibu/zoezi la upigaji kura liliendelea kama lilivyoelezwa na Msimamizi wa Uchaguzi na alieleza/alitoa taarifa kuwa Wabunge waliopo ni 280 ambao wametimiza akidi ya Wabunge 197.

(i) Kura zilipigwa kwa utaratibu maalum ulioelekezwa na kufafanuliwa na Msimamizi wa Uchaguzi na hatimaye kura zilikwenda kuhesabiwa.

(j) Hatimaye matokeo yalitangazwa ambapo washindi ni Josephine Sebastian Lemoyan na Pamela Simo Maassay kama walivyotangazwa na Msimamizi wa Uchaguzi kwa Mamlaka aliyonayo kwa Mujibu wa Sheria.

## XI. KUAHIRISHA BUNGE

Bunge liliahirishwa saa 3:50 hadi siku ya Alhamisi tarehe 11 Mei, 2017 saa 3:00 asubuhi.